**SEMINA YA WANAWAKE WALIOMALIZA VIFUNGO VYAO MAGEREZANI (WOMEN EX-PRISONERS) ILIYOFANYIKA KATIKA KITUO CHA NENDIWE – 12/11/2024**

**MTOA MADA: LUCAS MWIMO**

## MADA: KANUNI ZA KUFANIKIWA KATIKA UCHUMI BINAFSI

## UTANGULIZI

1. **Uchumi ni dhana pana inayohusisha, Uzalishaji mali na huduma (production of goods and services), Usambazaji mali na huduma (Distribution of goods and services), Utumiaji mali na huduma (Consumption of goods and services), na nyenzo za uzalishaji mali na huduma (factors of production). Kuna uchumi mkubwa (Macro-economy) ambao nchi nyingi huupima ukuaji wake kwa kutumia badiliko la kila mwaka la "Jumla ya thamani ya uzalishali wa mali na huduma katika sekta zote za uchumi – Gross Domestic Product (GDP)". Ili upate uchumi mkubwa lazima uanzie na ngazi ya uchumi wa mtu binafsi (Micro-economy). Katika semina hii tutaangalia uchumi wa mtu binafsi Micro-economy, ambapo tutajifunza kanuni mbali mbali zitakazomsaidia mtu kuwa na uchumi imara.**

2. **Uchumi wa watu wengi upo duni kutokana na kukosa ufahamu wa kutosha kuhusu kununi za kuwafanikisha katika shughuli zao za kila siku. Semina hii imelenga kukufundisha kanuni mhimu za kiuchumi/kifedha zitakazokuwezesha kufanikiwa na kustawi sana katika maisha yako. Ili uweze kufanikiwa katika uchumi binafsi zingatia kanuni zifuatazo;**

## KANUNI ZA KUFANIKIWA KATIKA UCHUMI WAKO
## KI-UNGU

1. **BADILISHA MTAZAMO WAKO NA MAWAZO YAKO JUU YA ZANA YA MAFANIKIO. Mtizamo ni picha ya ndani ya mtu juu ya jambo Fulani.**

    - **Upo jinsi ulivyo sasa kutokana na mawazo na maamuzi unayofanya kila siku.**
    - **Kushinda au kushindwa kwetu katika maisha hutegemea mawazo na maamuzi mbalimbali tunayoyafanya kila siku kwani kila kitu huanza na mawazo yetu.**
    - **Maisha yako hayawezi kuwa juu ya mawazo yako, bali maisha hufuata mawazo yako.**
    - **Aina ya mawazo na mtazamo inaamua hatima ya maisha utakayoishi, ama maisha ya utele, kawaida au umaskini.**
    - **Kataa mawazo ya kinyonge na mtazamo mbaya wa kushindwa**
    - **Ukitaka kufanikiwa na kuwa na uchumi bora, shikilia mtazamo wa ushindi, utele na utajiri katika mawazo yako. Jione kama Mungu anavyokuona kwani anataka ufanikiwe na uishi maisha ya utele na raha.**

2. **KUWA NA MAONO/NDOTO (VISION)**
   **Maono ni picha ya ndani juu ya maisha unayataka kuishi au kuyafikia mbeleni. Unataka kuwa nani na wapi miaka 5, 10, 20 etc ijayo?**
    - **Kama hauna picha ya maisha yako, hauna maisha na usipojua unapokwenda, utafika popote.**

- Mahali panapofurahisha ni maisha yale uliyoya-ZOOM ndani yako.
- Bila maono huwezi kuwa na mpango mkakati na malengo ya kile unachotaka kukifikia
- Asiye na maono hana maisha ya kufanikiwa.
- Kila mtu aliyefanikiwa, alianza kwanza kuwa na maono.
- Jitahidi uwe na picha ya maisha yako, jitahidi upajue unapo kwenda na hapo yalipo maisha na mafanikio yako.
- Moja ya sifa za watu wakuu walio fanya makubwa duniani na kuacha alama ni maisha ya maono.

Faida za kuwa na maono

- ✓ Maono yanakupa kuwajibika na kuukomboa wakati
- ✓ Maono yanakupa nidhamu- Kila mwenye maono lazima ajiwekee nidhamu ya nini cha kufanya na nini cha kutofanya ili kufikifia ndoto yake.
- ✓ Maono yanaamua wapi ufike- Kile unachoweza kukiona tu ndicho unaweza kukifikia. Maono yako yanapoishia ndipo na mafanikio yako yataishia.
- ✓ Maono yanakupa nguvu ya kufikia lengo
- ✓ Maono yanakupa kujiandaa vizuri kutekeleza malengo yako.

Amua leo, ishi kwa viwango vikuu kwa kuanza na picha ya maisha ya juu (ANZA KUWA NA MAONO LEO).

3. FANYA KAZI KWA BIDII, UBORA NA UAMINIFU. Fedha na utajiri hupatikana kupitia kufanya kazi na shughuli halali za kiuchumi. Ili ufanikiwe, fanya kazi/biashara na shughuli za kiuchumi kwa bidii na kwa Uaminifu.
   - Hakuna aliyefanikiwa katika maisha bila ya kufanya kazi kwa bidii. Kazi ni agizo la Mungu mwenyewe, asiyefanya kazi na asile - 2Wathesolonike 3:10.
   - Uaminifu katika kazi na huduma utainua uchumi wako binafsi. Uaminifu ni CV iliyo adimu katika jamii.
   - Tusifanye kazi bora liende bali kwa ubora. Kitakachokupa wateja na kibali ni ubora wa bidhaa unazozalisha. Kitakachokupa promotion kazini ni ubora wa kazi unazozifanya.

Biashara ni moja ya kazi za kuinua uchumi wetu hasa inapofanywa kwa kufuata kanuni za kiuchumi na biashara. Baadhi ya kanuni za kufanikisha biashara yako ni hizi hapa chini.

a. Fanya utafiti wa kutosha na kujirithisha kuwa biashara hiyo itakuletea faida.
b. Kuwepo kwa soko au wateja wa kudumu kununua bidhaa au huduma. Kwa biashara yoyote ile, kitu cha muhimu kabisa ni soko
c. Biashara iliyopo sehemu nzuri (convenient location). Kwa biashara za reja reja mahali ambapo panafaa ni penye watu wengi wanaopita.
d. Mpangilio mzuri wa bidhaa (Organized layout)
e. Bei za ushindani (competitive prices)- Angalia wenzako wanauzaje bidhaa kama zako. Hii pia inategemea uchaguzi mzuri wa maduka ya wholesale, au masoko etc.
f. Muuzaji makini, mchangamfu na anayesikiliza na kuwajali wateja “Mteja ni mfalme”. Hii itasaidia kujenga uhusiano mzuri kati yako na wateja wako. Ni lazima uwashawishi kwa nini waje kununua kwako na sio kwa wengine.
g. Usafi wa mazingira ya biashara na usafi wa muuzaji.

h. Usiuze vitu vilivyokwisha muda wake (vyakula). Ni vizuri ukavitupa na kuviteketeza.
i. Usijaze vitu (dukani) ambavyo utokaji wake ni mgumu kwani kwa kufanya hivyo utakalisha fedha yako na kupunguza faida.
j. Weka vivutio mbali mbali (e.g. Kupunguza bei ya vitu fulani hasa mteja anaponunua vitu vingi).
k. Matangazo ya utambulisho wa biashara yako yanayovutia wateja
l. Kopesha wateja waaminifu kwa uangalifu mkubwa, na hakikisha madeni yanalipwa mapema iwezekanavyo. Sio wateja wote ni waaminifu.
m. Jali muda wa wateja – fungua biashara yako kwa wakati unaotakiwa.
n. Wahudumie wateja wenye hasira/wakali kwa unyenyekevu na kushusha hasira zao.
o. Fanya maamuzi ya biashara yako kwa kuzingatia matakwa ya wateja wako. Kwa mfano kama wateja wanaulizia bidhaa hiyo hiyo na wewe hunayo, nenda ukaitafute.
p. Aina za bidhaa (variety). Weka aina nyingi za vitu ili kumwezesha mnunuzi anunue vitu vingi mahali pamoja.
q. Kwa vile vitu ambavyo stock imekwisha/imekaribia kwisha, replenish haraka na uwe mwaminifu kwa ahadi unazowapa wateja kuwa hadi tarehe fulani utakuwa umeleta bidhaa zilizokwisha.
r. Lipa kodi zote za Serikali na kuwa na leseni halali ya biashara yako.
s. Lipa wafanyakazi mishahara yao kwa wakati ili wasipate vishawishi vya kukuibia na kuwafanya kuipenda kazi yao.
t. Kuwa na daftari au system ya kutunza mahesabu. Mali bila daftari hupotea bila kujua. Faida kubwa ya kutunza kumbukumbu ni kukuwezesha kujua kama biashara unayoifanya ina faida au la hasha. Ukijua faida na kujilipa mshahara ndipo utaweza kulipa fungu la kumi na sadaka zingine.

## 4. KUWA NA NIDHAMU YA FEDHA NA KUBANA MATUMIZI (FINANCIAL DISPLINE)

- Mafanikio ya kiuchumi/biashara yanahitaji Nidhamu ya Fedha na Matumizi.
- Kinachofanya watu wengi washindwe kufikia ndoto za

mafanikio ya uchumi na maisha yao ni tatizo la matumizi mabaya ya fedha yasiyo na nidhamu.

- Sababu kubwa ya watu kutoweka akiba ni kutodhibiti matumizi. Ukishaweza kujizuia kwenye matumizi, tegemea utajiri.
- Matumizi ndiyo yanayoamua hatima ya utajiri au umaskini.
- Umaskini ni hali ya Matumizi yako kuwa makubwa kuliko kipato chako.
- Jifunze kuweka vipaumbele juu ya mahitaji muhimu utakayo fanya kwa pesa iliyopo mkononi mwako.
  - ✓ Usijaribu kutaka kutekeleza kila hitaji.
  - ✓ Mahitaji ni mengi hutaweza kuyamaliza.
  - ✓ Michango ni mingi hutaweza kumchangia kila mtu.
- Ishi maisha ya uhalisia na epuka matumizi ya fedha ili kuwaridhisha wanadamu pamoja na ndugu zako
- Moja ya kitu kitakachokusaidia kuwa na matumizi mazuri ni kuandaa bajeti na kuiheshimu.

Bajeti: Maana yake ni kuoanisha mapato na matumizi. Ni kupanga na kutawala matumizi. Kupanga bajeti ni kwa mhimu kama vile ilivyo muhimu kufanya kazi. Bajeti inayofanikiwa ni lazima izingatie mambo yafuatayo:

- Lazima itokane na mapato na sio mategemeo
- Ni lazima iwe ya kweli na ya utaratibu.
- Fedha ni lazima zipangwe kulingana na hitaji la kweli. Mume na mke ni budi wafanye pamoja kwa ajili ya kufanikisha bajeti yao. Bajeti inaweza kuwa ya wiki au ya mwezi kutegemeana na vyanzo vya mapato.
- Bajeti yenye mafanikio inahitaji utaratibu wa kutunza mahesabu kama vile kuwa na kitabu cha bajeti kuandika manunuzi yote, au bahasha zinazofichwa kwa usalama zenye fedha zote zilizopangwa au excel spreadsheet kwa wale wanotumia computers.
- Iwapo mapato hayamudu matumizi, ni budi pawepo na marekebisho ama kwa kupata mapato zaidi au kubana matumizi.

5. KUWA NA UTAMADUNI WA KUWEKA AKIBA (SAVINGS) – Lengo la kuweka akiba ni kupata fedha za dharura, kujiepusha na mikopo isiyokuwa ya lazima na kupata fedha ya mtaji kwa ajili ya uwekezaji.

    - Jifunze kuweka akiba kwa kila fedha unayoipata na kuiweka kwenye akaunti ya benki, Kibubu, Simu etc- Kila fedha inayoingia mikononi mwako ina mkate na mbegu (Akiba).
    - Usidharau akiba hata kama ni ndogo (Dangote ambaye ni moja wa matajiri sana Afrika alikuwa ameajiriwa na mjomba wake, akaanza kuweka akiba kidogo kidogo na sasa ni tajiri namba moja Africa)
    - Watu waliofanikiwa sana katika maisha ni wale waliojitahidi kujinyima na kujijengea mazoea ya kuweka akiba kidogo kidogo (Accumulation).
    - Tofauti ya Masikini na Tajiri ni kwamba Maskini akipata pesa anakula kwanza kisha anawekeza kama itakuwa imebakia. Tajiri akipata pesa anawekeza kwanza kisha anakula inayobaki.
    - Hakuna tajiri asiyeweka akiba. Mweka akiba yupo kwenye njia ya utajiri.
    - Tenga akiba kabla ya matumizi (kama 10% ya mapato yako). Akiba sio kile kilichobaki baada ya matumizi.
    - Itakukinga na madeni yasiyo ya lazima. Mtu asiyeweka akiba hawezi kukwepa madeni.

Adui mkubwa wa kuweka akiba ni kuahirisha. Ukiweza anza mwezi huu.

6. JIEPUSHE NA MADENI/MIKOPO

    Madhara ya madeni

- Madeni sio dhambi ila ni mzigo na utumwa unaotunyima pumziko. Lengo la madeni ni kukuletea masumbuko ya kiroho, kiuchumi, kiafya na kijamii. Madeni ni mzigo unaoelemea watu.
- Deni linasababisha uchovu, matatizo ya ndoa na hata kujinyonga.

- Deni linasababisha kufilisika na umaskini (mfano: Benki inapouza nyumba yako, na vitu vingine vya thamani ili kurejesha mkopo wake, mfano, mikopo ya VICOBA na SACCOs na Wakopeshaji binafsi wenye riba ya Kausha damu.
- Deni husababisha usongo wa mawazo na kupunguza uwezo wa ubunifu na kufikiri.

## SABABU AU VYANZO VIKUU VYA MIKOPO

1. Tamaa ya kuwa na vitu vingi kwa haraka –Tamaa ni kutoridhika na kile ambacho Mungu amekubariki kwa sasa. Wengi wapo kwenye madeni leo kwa sababu ya kung'ang'ania maisha yaliyo nje ya uwezo wao. Watu hukopa vitu maofisini hata kama havihitajiki kwa sasa, mfano magari na vitu vingi vinavyotolewa kwa mkopo.
2. Ufahari wa maisha – Kutaka ku-maintain status hata kama kipato kimepungua. Upo tayari kukopa ku-maintain status ili kuwafurahisha wanadamu. Ishi kwa hali halisi ya kipato chako bila kujali wanadamu watasema nini juu ya maisha yako.
3. Kuishi kufurahisha watu. Maisha yako ni kwa ajili ya Mungu sio wanadamu. Wengi wameingia kwenye madeni kwa ajili ya kufurahisha wengine.
4. Kutegemea chanzo kimoja tu cha kipato, mfano mshahara.
5. Kutokuwa na utamaduni wa kuweka akiba.

## MBINU ZA KUJIEPUSHA NA KUTOKA KWENYE MADENI

1. Usikubali mkopo ukawa kianzio cha chochote unachotaka kuanza cha kiuchumi. Sio hekima kuanza kitu kipya kwa mkopo. Moja ya sababu kubwa ya madeni ni watu kukopa kuanzisha miradi bila kufanya utafiti na mchanganuo wa mradi kwa makini kuona kama biashara itakuwa na faida au la.
   Wenye hekima hukopa ili kuendeleza biashara ambazo tayari zinaleta faida kubwa wala sio kuanzisha miradi.

2. Tambua nguvu ya kidogo ulicho nacho. Mungu anataka uanzishe mradi na fedha zako hata ukianza na mtaji mdogo. Kidogo cha kwako ni bora zaidi kuliko kikubwa cha kukopa.

3. Usiruke hatua ya maisha huku ukimsubiri Mungu kukuvusha kwenye hatua nyingine. Maisha yapo kwenye hatua. Watu wengi walio kwenye mikopo ni watu walioruka/wanaotaka kuruka mchakato wa maisha. Siku hizi masharti ya mikopo yapo rahisi na ushawishi ni mkubwa ili uingie kwenye mikopo—KATAA. Kila unapokopa haujatatua bali umetatiza maisha.
4. Kataa maisha ya kutamani kila kitu, ridhika na ulicho nacho huku ukimsubiri Mungu.
5. Acha maisha ya mashindano. Kuna mtu leo yupo kwenye madeni kutokana na maisha ya mashindano.
6. Jiepushe kumdhamini mtu kwa ajili ya mkopo - Kumdhamini mtu kwa ajili ya mkopo ni njia hatari ya kujichafua na deni na huleta uangamivu wa kifedha. Unapodhamini, wewe unawajibika kwa lile deni sawa sawa na yule anayepokea zile fedha.
7. Panga kwa utaratibu na mpangilio jumla ya madeni yote uliyonayo na watu wanaokudai kisha wasiliana nao na kukubaliana namna ya kuyalipa.

8. Uza baadhi ya vitu ulivyonavyo ili kulipa deni.

7. KUWA NA CHANZO ZAIDI YA KIMOJA CHA KUKUINGIZIA MAPATO/FEDHA.

Anzisha chanzo kingine cha mapato kwa kutumia akiba

- Kataa kutegemea mshahara pekee kama chanzo cha mapato. Mshahara ni mbegu tu haiwezi kukufanya kuinuka kiuchumi, ukiutegemea utaishia kuishi maisha ya wastani.
  - Kutegemea mshahara tu ni kualika madeni ktk maisha yako.
  - Chukua hatua ya kuwekeza hata kwa kidogo ulicho nacho baada ya kufanya utafiti.
  - Mungu huvutiwa na watu wanaodhubutu
  - Wengi wa waliofanikiwa leo, walianza na kidogo

MAENEO YA UWEKEZAJI

Wekeza ktk sekta mbali mbali ili kuepuka kuwa na chanzo kimoja cha mapato (Diversification)- Mwanzo 2:10-14

1. Hati fungani za Serikali -Dhamana za Serikali (Treasury bills (za muda mfupi) and Bonds –za muda mrefu 5-25 years. 25 Years with 15.95% interest).
2. Kununua Hisa kwenye makampuni mbali- mbali (Hisa zinauzwa katika soko la mitaji la DSM Stock Exchange kupitia brokers). Kuwa mwangalifu katika kununua hisa kama za TBL na Sigara ambazo sisi tuliookoka hatupaswi kujichafua nazo licha ya kuwa na faida kubwa.
3. Wekeza kwenye Mifuko maalumu ya fedha: Unit Trust of Tanzania (UTT-Ukwasi (11% -12%), INUKA (imeanzishwa miezi 2 iliyopita na inahusisha nchi zingine za Afrika Mashariki, FAIDIKA (mifuko binafsi).
4. Biashara ya fedha za kigeni – Ukiacha Bure de change ambazo hufanya biashara ya fedha za kigeni kwa kufuata sheria za nchi husika, kuna biashara za fedha za kigeni zinazofanywa kwa njia ya mitandaoni baada ya mhusika kupewa kwanza platform na mawaka (brokers).
   Fedha zinazouzwa kwenye platform hizi ni
   (i) Cryptocurrency exchange mainly bitcoin- Hizi ni fedha za kimtandao. Bado hakuna sheria za BOT zinazosimamia biashara hii hivyo kila anayejihusisha na biashara hizi za mitandaoni ni kwa hasara yake mwenyewe na hatakuwa na sehemu yeyote ya kushitaki endapo fedha yake itadhulumiwa.
   (ii) Fedha za kigeni (mfano: USD, YEN, etc). Biashara hii inahitaji elimu na ujuzi wa hali ya juu hasa kuelewa mwenendo wa masoko ya fedha duniani na hali ya uchumi wa dunia. Kama huna ujuzi huo usijiingize kwenye biashara hii utapoteza fedha yako.

5. Fixed deposits accounts kwenye mabenki ya biashara kwa mapatano ya riba watakayokulipa kwa mwaka. Kwa sasa riba ni kati ya 11-13% kwa baadhi ya mabenki.
6. Kuanzisha taasisi ndogo za fedha za kukopesha (sio zile za mfukoni zenye riba ya kukausha damu).

7. Kuweka fedha kwenye VICOBA, SACCOs ambazo kama una biashara yenye faida unayoifanya unaweza kukopa kwa kuiendeleza. Riba zao zipo chini sana.
8. Maeneo mengine ya kuwekeza kwa biashara ndogo ndogo na za kati ni, Hard ware, Supermakets, Maduka ya dawa, Maduka ya rejareja na jumla, Kujenga nyumba za kupangisha, hotel, kulipa, kununua viwanja na kuviuza n.k. kutegemea na utafiti na ujuzi wa mtu husika. Biashara ndogo ndogo zipo nyingi siwezi kuzitaja zote hapa.

## 8. KATAA HOFU NA KUKATA TAMAA UNAPOONA UCHUMI WAKO UMEANGUKA AU HAUENDI VIZURI.

- ✓ Hofu ni mwizi wa maongezeko
- ✓ Anguko lisipite na maisha yako. Anguko likupe uzoefu wa kufanya vizuri tena baada ya kuanguka
- ✓ Hofu ni mlango ambao adui/shetani anautumia ili kumtesa mwanadamu.
- ✓ Hofu huondoa tumaini na nguvu ya imani

## 9. KUPUNGUZA MARAFIKI

- Kesho ya mtu kiuchumi inaweza kuamuliwa na aina ya marafiki wanaomzunguka leo. Marafiki wanaweza kukupunguzia au kukuchelewesha mwendo wa kupata mafanikio kwa haraka
- Kuchagua aina ya marafiki wa kuambatana nao ni kuamua kesho yako iweje wala sio kiburi wala kukosa upendo.
- Marafiki wanaweza kuathiri tabia yako
  - Kuwa na marafiki wanaokupa changamoto au wenye ndoto za kufanikiwa.
  - Sio kila rafiki ana maono kama yako na hivyo hatakuwa na mchango wowote katika ambatano lenu
  - Sio kila rafiki ana upendo wa kweli. Marafiki wenye upendo wa kweli ni wachache
  - Baadhi ya marafiki wanaweza kukusaliti
  - Ule usemi unaosema "niambie rafiki yako nikwambie tabia yako" Kuwa na marafiki wengi husababisha kutokufikia ndoto zako au mafanikio unayoyahitaji. Jiulize maongezi yenu huwa yanahusu nini zaidi? Kuna unachojifunza chochote kulingana na maongezi yenu ya kila siku?
  - Epeka marafiki wasio na maono, wakatisha tamaa, wasiomcha Mungu, Wasio omba, wapenda anasa, wapoteza muda, waseng'enyaji, wenye mizaha na waovu (walevi, waongo, wazinzi, watukanaji, wanafiki)

## 10. KUKATAA MAISHA YA UOVU

Maisha ya uovu ni kikwazo kikubwa kwa watu wengi kufanikiwa kiuchumi na kupoteza fedha ambazo zingewafanya kuwa matajiri.

- Kukataa uovu ni kutunza uhusiano mzuri na Mungu na Mungu atakusaidia katika maeneo yote ya maisha yako

**11. KOMBOA WAKATI** (kutumia muda wako vizuri). Maana ya kuukomboa wakati ni kuutumia muda vizuri ambao Mungu ametupatia bure.

- ✓ Umewahi kusikia watu wakisema “time is money.” Hii ina maana kuwa muda ni wa thamani sana katika maisha ya mwanadamu. Linapokuja suala la kutaka kufanikiwa katika jambo lolote lile katika maisha ya kiroho na kimwili, muda ndio suala la muhimu sana kuzingatia kuliko jambo lingine.
- ✓ Watu wengi hufikiri mafanikio yanahitaji fedha tu peke yake, kumbe mafanikio pia yanahitaji matumizi sahihi ya muda kwa ajili ya kukamilisha ndoto tulizonazo. Ni muhimu kufahamu ya kwamba muda ukishapita kama hujautumia vizuri hautarudi tena, muda una mipaka.
- ✓ Muda uliopotezwa ni maisha yaliyopotezwa kwa sababu maisha ya mtu yamefungwa kwenye muda. Usipofanya yanayokuhusu kwa wakati na majira yake, tegemea kuchelewa sana au kutofikia kabisa hatima ya maisha yako.
- ✓ Uwe na kiasi cha kutumia mitandao ya kijamii ambayo hupotezea watu muda mwingi ukilinganisha na faida zinazotokana na mitandao hiyo. Tumia mitandao ya kijamii kwa faida tu, vinginevyo itakupotezea muda mwingi ambao ungeutumia kufanya vitu vingine vyenye faida.

12. **TUNZA AFYA YAKO** –Afya ni mtaji mkubwa sana katika kufanikiwa. Afya na uhai ni baraka kuu toka kwa Mungu. Pamoja na kumwomba Mungu kutulinda na kutuepusha na magonjwa, tunawajibika kutunza afya zetu kwa kufuata na Kuzingatia kanuni au sheria za afya, Mfano Kula chakula bora, Kufanya mazoezi, Kunywa maji mengi, kupata Mwanga wa jua, Kuwa na kiasi katika mambo yote, Kuvuta hewa safi, Kupumzika na Kumtegemea Mungu.

++++++++++++MWISHO WA SEMINA+++++++++++++++++++